

**TANGAZO LA KUFUNGA VITUO VYA KULELEA  
WATOTO WADOGO MCHANA (DAY CARE CENTRE)  
JANUARY 2021.**

1. MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA ANAWATANGAZIA WANANCHI KUWA KUTAKUWA NA ZOEZI LA KUFUNGA VITUO VYOTE VYA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA VISIVYOSAJILIWA KWA MUJIBU WA SHERIA.
2. ZOEZI HILI LINALENGA KUBORESHA UTOAJI WA HUDUMA YA MALEZI KAMA ILIVYOAINISHWA KATIKA SHERIA YA MTOTO NA. 21 YA MWAKA 2009 ILIYOFANYIWA MAREKEBISHO AMBAYO INAELEKEZA TARATIBU ZA UANZISHAJI WA VITUO HIVYO.
3. KWA MUJIBU WA SHERIA HII, NI KOSA LA JINAI KUWEKA WATOTO WADOGO BILA YA KUPEWA KIBALI CHA KUENDESHA KITUO NA MAMLAKA HUSIKA. KIFUNGU 155 (a), (b) NA (c) CHA SHERIA YA MTOTO NA 21(2009) INAELEKEZA MAKOSA NA ADHABU AMBAPO FAINI YAKE ISIYOPUNGUA TSHS. 2,000,000.00 (milioni mbili) NA ISIZOZIDI TSHS. 5,000,000.00 (milioni tano) AU KIFUNGO KISICHOZIDI MWAKA MMOJA AU VYOTE KWA PAMOJA, ATALIPA FAINI YA ZIADA YA TSHS. 100,000(LAKI MOJA) KWA KILA SIKU AMBAYO KOSA LINAENDELEA KUFANYIKA.
4. KWA TANGAZO HILI UNASHAURIWA KUSAJIRI AU KUFUNGA KITUO CHAKO MARA MOJA KABLA YA HATUA STAHIKI ZA KISHERIA HAZIJACHUKULIWA DHIDI YAKO.

N:B MWANANCHI UNATAARIFIWA KUPELEKA MTOTO WAKO KATIKA VITUO VYA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA (DAY CARE CENTRE) VILIVYOSAJIRIWA NA MAMLAKA HUSIKA, UKIPATA TAARIFA HII MPE TAARIFA MWENZIO KUEPUKA USUMBUFU UTAKAOJITokeza.

 MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
KYELA

EZEKIEL H. MAGEHEMA  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)